JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA TARIME

Simu Na.: +255 28 2690218
Nukushi: +255 28 2690218
Barua pepe:td@tarimetc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji
S.L.P 45,
TARIME

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. HMT/L:I/3VOL IV/140

14 /02/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA KATIKA ZOEZI LA MRADI WA KUPANGA,KUPIMA NA KUMILIKISHA ARDHI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tarime anawatangazia Wananchi wote wenye sifa na ambao ni Raia wa Tanzania kuomba nafasi za kazi ya muda (Mkataba) ambao watashiriki katika zoezi la mradi wa kupanga,kupima na kumilikisha kama ifuatavyo:-

1. WAPIMA ARDHI WASAIDIZI (ASSISTANT SURVEYORS)-NAFASI 8

Sifa:

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na elimu ya kidato cha IV au VI na amehitimu Astashahada/Stashahada kutoka katika chuo kikuu kishirikishi cha ardhi na usanifu majengo katika fani ya upimaji ardhi au taasisi yoyote inayotambuliwa na national council of professionals surveyors (NCPS)
iii. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

Kazi na Majukumu.

i. Kuingiza taarifa za upimaji kwenye kompyuta.
ii. Kukagua kazi za upimaji na kuingiza taarifa za kazi zilizothibitishwa kwenye kompyuta.
iii. Kufanya upimaji picha.
iv. Kuandaa vikosi kwa ajili ya kuhuisha ramani.
v. Kutunza kumbukumbu za picha za anga.

Scanned by TapScanner

2. AFISA MIPANGO MIJI- NAFASI 1

Sifa:

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na elimu ya kidato cha IV au VI na amehitimu stashahada ya juu/shahada katika fani ya mipango miji kutoka chuo kikuu kishirikishi cha ardhi na usanifu majengo(UCLAS) au vyuo vikuu vingine vinavyotambuliwa na serikali.
iii. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

Kazi na Majukumu.

i. Kuandaa mipango ya maeneo yaliyoendeleza kiolela.
ii. Kuandaa michoro ya mipangomiji.
iii. Kuchambua takwimu na taarifa kwa ajili ya maandalizi ya mipango mipya ya makazi.
iv. Kupokea nakuweka kumbumbuku za maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi na umegaji wa viwanja.
v. Kuhakikisha kuwa mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanaingizwa katika michoro.

3. AFISA ARDHI MSAIDIZI(ASSISTANT LAND OFFICER)-NAFASI 4

Sifa:

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na elimu ya kidato cha IV au VI na amehitimu mafunzo ya cheti ya usimamizi wa ardhi na uthamini kutoka vyuo vya ardhi ,vyuo vya sheria au vyuo vinginevyo vinavyotambuliwa na serikali.
iii. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

Kazi na Majukumu.

i. Kuingiza kumbukumbu katika kompyuta.
ii. Kutoa ushauri kwa wateja
iii. Kusaidia Maafisa Ardhi katika ukaguzi na kuchukua kumbukumbu kama picha,taarifa,vipimo vya majumba na michoro.
iv. Kujumuisha na kuandaa taarifa za ukaguzi.
v. Kuandaa rasimu za Hati na uingizaji wa plani ya Hati (deed plan).

4. MPIMA ARDHI II (LAND SURVEYORS)-NAFASI 2

Sifa:

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na Stashahada ya juu au Shahada katika fani ya upimaji Ardhi ktoka Taasisi inayotambuliwa na National Council of Professional Surveyors (NCPS).
iii. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

Scanned by TapScanner

Kazi na Majukumu.

i. Kuingiza taarifa za upimaji.
ii. Kukagua kazi za upimaji na kuingiza taarifa za kazi za upimaji kwenye kompyuta.
iii. Kufanya upimaji wa picha.
iv. Kuhuisha ramani za upimaji.

5. WAKUSANYA MAPATO (REVENUE COLLECTORS)-NAFASI 6

Sifa:

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na elimu ya kidato cha IV au VI na amehitimu Astashahada katika fani za Utawala /Utumishi , Sheria, Mipango/Uchumi, Maendelo ya Jamii, kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
iii. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

Kazi na Majukumu.

i. Kukusanya mapato yote yaliyopo kwa mujibu wa sheria za nchi ndani ya Halmashauri ya Mji Tarime.
ii. Kutoa risiti kwa mlipaji wa mapato kukiri kupokea fedha.
iii. Kukusanya mapato kwa uaminifu na uadilifu mkubwa bila kuingiza maslahi binafsi yatakayopingana na maslahi ya Halmashauri.

6. WAKUSANYA TAKWIMU (DATA CLERK) – NAFASI 14

Sifa.

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na elimu ya kidato cha IV au VI na amehitimu Astashahada katika fani za Utawala /Utumishi , Takwimu, Mipango/Uchumi, Maendelo ya Jamii, kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
iii. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

Kazi na Majukumu.

i. Kuandaa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu
ii. Ukusanyaji ,uchakatuaji na uchambuzi wa takwimu
iii. Kuchagua na kuthibitisha usahihi wa taarifa kabla ya kuziingiza kwenye mfumo
iv. Kuweka na kusahihisha makosa na kutoa taarifa kwa msimamizi.
v. Kuchagua vifaa vinavyohitajika kukamilisha kazi husika.
vi. Kuhifadhi nyaraka zilizokamilika katika maeneo sahihi na kuzikabidhi kwa muingiza kumbukumbu.

Scanned by TapScanner

7. MUINGIZA KUMBUKUMBU(DATA ENTRY)-NAFASI 2

Sifa

i. Awe Raia wa Tanzania.
ii. Awe na elimu ya kidato cha IV au VI na amehitimu Astashahada katika fani za Utawala /Utumishi,Takwimu ,Mipango/Uchumi, Maendelo ya Jamii, kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
iii. Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za Windows, Microsoft office, Internet, E-mail na Publisher.
iv. Awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

Kazi na Majukumu.

i. Kutumia kompyuta na programu za uchakatuaji wa takwimu ili kuziingiza taarifa kwenye kihifadhi takwimu (database).
ii. Kuhamisha data kutoka kwenye muundo wa karatasi na kuzirekodi kwenye kihifadhi takwimu (database).
iii. Kuunganisha twakwimu kutoka kwenye mifumo yote pale ambapo taarifa husika hazijakamilika.
iv. Kutunza nyaraka za muundo wa karatasi kuepusha upotevu wa takwimu .
v. Kuchangia juhudi za kazi ya pamoja kwa kutimiza matokeo yanayohusiana pale inapohitajika.

MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA:

i. Waombaji wawe wa umri kati ya mika 18 – 40.
ii. Waombaji wote waambatanishe vivuli vya vyeti vyao na kwenye barua za maombi pia waandike namba zao za simu.
iii. Barua zibandikwe picha mbili (Stamp Size).
iv. Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P 45,
TARIME.

v. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24.02.2022 saa 9:30 alasiri maombi yatakayowasilisswa baada ya tarehe tajwa hayatapokelewa.

Gimbana E. Ntavyo
MKURUGENZI WA MJI
TARIME

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA MJI WA
TARIME

Scanned by TapScanner